**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 7, Issue 1, 2024**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Usawiri Wa Vyanzo Vya Dhuluma Za Kijinsia Katika Riwaya Teule Za Kiswahili

*Pamella Tsiyeli Ngeleso[1*] & Alex Umbima Kevogo[2]*

[1] Chuo Kikuu cha Mount Kenya, S. L. P. 342-01000, Thika, Kenya.
[2] Chuo Kikuu cha Garissa, S. L. P. 1801 – 70100, University Way, Garisa, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: alumasapam04@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2024**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*05 Julai 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Usawiri, Dhuluma za Kijinsia, Riwaya Teule.*

**IKISIRI**

Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya 2020 inatoa takwimu za kusikitisha kuhusu idadi ya waathiriwa wa dhuluma za kijinsia duniani. Data hii ilichochea utafiti huu kuhusu dhuluma za kijinsia na zinavyosawiriwa katika kazi za fasihi. Kimsingi utafiti huu ulikuwa wa maktabani; ambapo watafiti walisoma na kuhakiki riwaya teule za ‘Nyuso za Mwanamke’ ya Said Ahmed Mohamed na ‘Unaitwa Nani?’ ya Kyalo Wadi Wamitila. Uteuzi wa sampuli wa kimakusudi ulitumika ili kuchagua riwaya moja ya kila mwandishi kwa mujibu wa mada ya dhuluma za kijinsia. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Ufeministi Mamboleo iliyoasisiwa na Jacques J. Zephire mwaka wa 1982. Aidha, utafiti huu ulizingatia pia Nadharia ya Hegemonia ya Ubabedume iliyoasisiwa na Raewyn Connell mnamo 1987. Kimsingi, utafiti huu ulilenga kubainisha vyanzo vya dhuluma ya kijinsia na namna vinavyosawiriwa katika riwaya ‘Nyuso za Mwanamke’ na ‘Unaitwa Nani?’. Matokeo ya utafiti yanayohusu data ya kiuthamano yaliwasilishwa kupitia kwa maelezo na ufafanuzi unaotolewa kwa kuegemea mihimili ya Nadharia ya Ufeministi Mamboleo na Nadharia ya Hegemonia ya Ubabedume. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa riwaya hizi zinasawiri wahusika mbalimbali wanaokuza maudhui ya dhuluma ya kijinsia. Utafiti huu utawafaa wahakiki wengine wa kazi za fasihi kupata maarifa mapya yanayohusu masuala ya kijinsia. Aidha, wanaharakati wanaopambana na suala la dhuluma za kijinsia watapata mapendekezo ya waandishi na watafiti kuhusu njia za kupambana na tatizo hili. Isitoshe, serikali na vyombo visivyo vya kiserikali vinavyoshughulikia suala la dhuluma za kijinsia vitashauriwa kuhusu njia mwafaka za kudumisha utangamano na mahusiano ya kijinsia duniani, Afrika, Afrika Mashariki na hata nchini Kenya.

**APA CITATION**

Ngeleso, P. T. & Kevogo, A. U. (2024). Usawiri Wa Vyanzo Vya Dhuluma Za Kijinsia Katika Riwaya Teule Za Kiswahili. *East African Journal of Swahili Studies, 7*(1), 308-318. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2024.

**CHICAGO CITATION**

Ngeleso, Pamella Tsiyeli and Alex Umbima Kevogo. 2024. “Usawiri Wa Vyanzo Vya Dhuluma Za Kijinsia Katika Riwaya Teule Za Kiswahili”. *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 308-318. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2024.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2024

**HARVARD CITATION**

Ngeleso, P. T. & Kevogo, A. U. (2024) "Usawiri Wa Vyanzo Vya Dhuluma Za Kijinsia Katika Riwaya Teule Za Kiswahili", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 308-318. doi: 10.37284/jammk.7.1.2024

**IEEE CITATION**

P. T. Ngeleso & A. U. Kevogo "Usawiri Wa Vyanzo Vya Dhuluma Za Kijinsia Katika Riwaya Teule Za Kiswahili", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 308-318, Jul. 2024.

**MLA CITATION**

Ngeleso, Pamella Tsiyeli & Alex Umbima Kevogo. "Usawiri Wa Vyanzo Vya Dhuluma Za Kijinsia Katika Riwaya Teule Za Kiswahili". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Jul. 2024, pp. 308-318, doi:10.37284/jammk.7.1.2024.

## UTANGULIZI

Dhuluma za kijinsia zinaendelea kuongezeka duniani, Afrika na hata nchini Kenya. Sababu za dhuluma hizi zinaweza kuwa uchangamano na utangamano wa binadamu wenye hulka mbalimbali. Tunapoangalia kwa makini, tunatanabahi kuwa dhuluma za kijinsia ni tatizo sugu kwa maana limekuwepo, lipo na linaendelea kukita mizizi katika jamii ya kisasa (WHO, 2020). Wanaotekeleza dhuluma hizi kwa wenzao wanaweza kuwa jamaa zao au watu wasiowajua. Baadhi ya vyanzo vya dhuluma hizi vinaweza kuwa tamaa zilizokithiri, kutowajibika kwa wanajamii, umaskini na kuzuka kwa majanga na milipuko ya magonjwa sugu kama Corona (Covid-19). Athari za dhuluma za kijinsia zinazodhihirika bayana katika jamii ya kisasa ni mauaji katili ya wanandoa na watoto, ulemavu, ongezeko la msongo wa mawazo, magonjwa sugu, vita, kuvunjika kwa ndoa, umaskini na hata ukosefu wa elimu miongoni mwa watoto wa familia zilizoathirika.

Utafiti huu ulilenga kushughulikia vyanzo vya dhuluma za kijinsia, athari ya dhuluma ya kijinsia na kupendekeza suluhu kwa matatizo haya. Taasisi inayoshughulikia Dhuluma za Kijinsia nchini Kenya inatazamia katika malengo yake, kuikabili changamoto hii kufikia mwaka 2030. Hali hii inapaswa kuchunguzwa kwa dharura ili kubaini vyanzo, athari na suluhu za dhuluma za kijinsia ili kuihamasisha jamii jinsi ya kulikabili na kulimaliza tatizo hili. Pia, dhuluma za kijinsia likiwa suala tatizi, limejitokeza katika sura na nyuso mbalimbali zinazotamausha jamii ya kisasa.

### Dhuluma ya Kijinsia katika Fasihi ya Kiswahili

Mayieka (2015) akimrejelea Khamis (2012) anaeleza kuwa, riwaya ya kisasa inaangazia matatizo halisi yanayoikabili jamii ya kisasa katika viwango vya kitaifa na kimataifa yakiwemo ufisadi, uongozi wa kiimla, ubaguzi, ukiukwaji wa maadili, tamaa, kutowajibika kazini, ukiukwaji wa haki za kibinadamu pamoja na migogoro ya kimapenzi na ndoa miongoni mwa mengine. Matatizo haya ndivyo vyanzo vya dhuluma katika jamii. Hali hii ilichochea ari yetu ya kutaka kutafiti kuhusu vyanzo vya dhuluma za kijinsia katika jamii ya Kiafrika pamoja na suluhisho la changamoto hii maishani.

Utafiti wa Mboya (2018) unabainisha vyanzo vya dhuluma kwa mwanamke katika jamii inayotawaliwa na ubabedume na kumwona mwanamke kuwa dhaifu na mtegemezi. Vyanzo vya ubabedume vinaonekana katika mifumodume iliyoshenezwa katika asasi mbalimbali za jamii hususan dini, siasa, utamaduni na uchumi. Hali hii humtenga na kumbagua mwanamke na kumfungia katika ngome ya upweke na uhitaji. Hali hii inamfanya mwanamke kuonekana duni na hohehahe katika himaya inayotawaliwa na mwanamume. Mwanamke anahamasishwa kujikomboa na kujikwamua kutoka kwa dhuluma na ukandamizwaji huo.

Nyangweso (2017) anaangazia nafasi dhalilishi ya mwanamke katika jamii. Utafiti huu unabainisha jinsi mwanamke alivyodharauliwa na kuteswa, kutosikizwa, kuonewa, kufanywa chombo cha mapenzi, uzazi na malezi pamoja na kudhulumiwa kimabavu anapopigania haki yake. Hali hii imewachochea wanawake kupata mwammko mpya wa kujizatiti kupigania haki yao

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2024

na kujikomboa kutoka kwa dhuluma zinazowakabili ili kujenga jamii mpya. Kwa upande wake, Kibigo (2020) anachunguza ubabedume unavyobainika katika majigambo. Mtafiti huyu anabainisha kuwa mfumodume unampendelea mume na kumfanya kuwa mmiliki wa mali katika jamii. Hili huhimiliwa na utamaduni unaomhitaji mwanamume kutoa mahari kwa mkewe na hivyo kumfanya mke kuwa mali ya mwanamume. Hali hii humkosesha mwanamke nafasi ya kujieleza na kunyimwa uhuru wake.

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Ufeministi Mamboleo. Tapo la Ufeministi Mamboleo lilizuka miaka ya 1980 na kufafanuliwa zaidi na Jacques J. Zephire. Ufeministi Mamboleo ni tapo linalotokana na wimbi la Ufeministi wa pili ambalo linampa mwanamke nguvu, uwezo na hadhi kwa kusherehekea sifa zake ya kuwa mwanamke. Isitoshe, utafiti huu unatumia Nadharia ya Hegemonia ya Ubabedume iliyoasisiwa na Raewyn Connell mnamo 1987 kuchunguza vyanzo vya hegemonia ya ubabedume katika jumuia zinazosawiriwa katika riwaya zinazochanganuliwa katika utafiti huu. Connell (1987) alianzisha dhana ya 'Hegemonia ya Ubabedume' kueleza uhusiano wa nguvu, uwezo na mamlaka uliopo baina ya wanaume na wanawake katika jamii.

## Vyanzo vya Dhuluma ya Kijinsia katika Riwaya Teule

Utafiti huu ulibainisha kuwa waandishi wa riwaya mbili zinazochunguzwa wamasawiri dhuluma za kijinsia kuwa na vyanzo vyake katika misingi ya jamii kiutamaduni, kisiasa, kiuchumi na kidini.Sehemu inayofuata inafafanua jinsi waandishi wa riwaya za *'Nyuso za Mwanamke'* na *'Unaitwa Nani?'* wanavyosawiri vyanzo vya dhuluma za kijinsia kwa kuzingatia mkabala linganishi.

### Dhuluma za Kijinsia zinazotokana na Utamaduni

Kila jamii huwa na mila na desturi zake zinazoongoza jinsi wanajamii wanavyofanya na kutekeleza mambo na hata mwonoulimwengu wao. Desturi hizi huwapokonya baadhi ya wanajamii uhuru na usawa wao na hivyo kuendeleza dhuluma. Katika riwaya ya *'Nyuso za Mwanamke'*, baadhi ya wanawake wanachaguliwa wachumba na wazazi wao bila kuruhusiwa kutoa maoni wala kuchangia katika maamuzi hayo. Kwa mfano, Nana anachaguliwa mume na babake kwa kuegemea utabaka kwani familia hizo mbili zilikuwa tajiri na za tabaka la juu; hata hivyo ndoa hiyo haikutimilika. Hali hii inabainika wazi Nana anapotoa rai kuwa:

'.... Dusa ni kijana mwenzangu ndiyo, lakini sikumchagua. Nimechaguliwa na babangu awe mchumba wangu na hatimaye mume wangu. Dusa ni kijana mtukutu. Babake ni kizito mwenzetu ndiyo, lakini..' *Nyuso za Mwanamke*, Uk. 44

Licha ya kuwa Dusa alikuwa kijana wa kitajiri, Nana hakumpenda na hivyo kukataa maamuzi ya babake ya kumchagulia mume. Hali hii inazua mgogoro baina yao na hata Nana anazabwa kibao na babake. Hili linabainisha kuwa mfumodume wa ndoa ya kitamaduni unampa baba hadhi ya kumchagulia bintiye mchumba hata bila kumuuliza iwapo anaridhia uteuzi huo. Nana anaonekana kuwa na urazini wa kiakili kuhusu kaki yake ya kujichagulia mchumba. Nadharia ya Ufeministi Mamboleo inapinga dhana ya kuteuliwa mchumba na kuweka kumpa mke huru wa kujiamulia. Nadharia hii inapinga mfumodume wa kuwapa wanaume kipaumbele katika masuala ya uamuzi unaoomhusu mwanamke hususan uteuzi wa mchumba. Hali hii ndiyo inayozua mgogoro baina ya Nana na babake kwani baba anaona kuwa ana uwezo na mamlaka juu ya mtoto wa kike kupitia kwa mila na desturi. Utamaduni unamdunisha mke na kumwona kama asiyeweza kujitawala wala kujiamulia. Nana anazabwa kibao anapoonekana kukiuka hali hii na kutaka kujichagulia ampendaye. Matumizi ya mabavu kushinikiza uamuzi ulioidhinishwa na utamaduni dhalimu yanatokana na mfumodume unaompa mume idhili ya kumdhulumu mwanamke. Hata hivyo Nana anasimama kidete na kupigania uhuru na haki yake wa kujichagulia mchumba maishani. Mwandishi anapendekeza

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2024

kuwa, iwapo uhuru wa mwanamke utakiukwa kwa kutaka kumyamazisha kwenye uamuzi unaohusu mustakabali wake, ni vyema atumie sauti yake kujieleza kwa mapana na marefu hadi asikizwe kwa kuwa sauti yake ndiyo nguvu yake imara na ndicho chombo muhimu cha kujenga jamii mpya isiyo na dhuluma.

Utamaduni pia umesawiriwa kuwa chanzo cha kumkandamiza mwanamke kwa kusisitiza hali ya kuoza mabinti kwa lazima. Wazazi wanaona kuwa ni wajibu wao kuwaoza watoto wa kike. Isitoshe watoto wa kike wanachukuliwa kama bidhaa zinazomilikiwa na wazazi. Dondoo lifuatalo linaakisi hali hiyo:

‘...tokea zamani watoto wa kike walikuwa wakiozwa waume kwa nguvu. Tokea zamani wazazi waliona bora waondoe bidhaa mbovu njiani.’ *Nyuso za Mwanamke*, uk. 210

Katika jamii inayosawiriwa katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, wazazi wengi wanakuwa hofu kuhusu watoto wa kike kupata mimba kabla ya kuozwa na hivyo kuamua kuwaoza kwa nguvu bila kujali wanakiuka haki yao mradi tu wawaondokee. Pia, wanatazamia kuwa watoto wao wa kike wataolewa katika jamii fulani na hivyo kuwanyima fursa ya kujichagulia wachumba. Hili linaendeleza dhuluma za kijinsia kwani ndoa nyingi zinavunjika kwa kuozwa kwa watu wasiowapenda. Nadharia ya ufeministi mamboleo inahimiza uhuru wa kujiamulia kama haki ya kimsingi ya mwanamke.

Kwa upande mwingine, katika riwaya ya *‘Unaitwa Nani?’* tunabaini taswira tofauti kwani mwanamke anasawiriwa akiwa na nafasi ya kufanya maamuzi kuhusu mume atakayemuoa. Kwa mfano. Hali hii inadhihirika katika dondoo lifuatalo:

‘Miezi michache baadaye nilifika nyumbani na mjomba, Kiseku, kuniambia kuwa Agusto alitaka kusema nami. Nami? Mjomba akasema, ndiyo. Nilishangaa... alitaka kuniposa.’ *Unaitwa Nani?* Uk 42

Sehemu hii inadhihirisha kuwa mwanamke alipewa nafasi ya kuteua mwanandoa mwenzake kama ilivyo kwa Kasekesi anapopewa ujumbe na mjomba wake kuwa Agusto alitaka kusema naye bila kumdokezea hoja anayotaka kumwambia. Nadharia ya Ufeministi Mamboleo inatambua haki ya mwanamke kujifanyia uamuzi unaoathiri maisha yake jinsi ilivyo katika hali inayomkabili Kasekesi.

Tunaporejelea ushauri wa mama kwa Kasekesi kupitia kwa mbinu rejeshi, tunabaini kuwa mwanamke aliruhusiwa kujichagulia mchumba au hata kufanya uamuzi kutoolewa. Taswira hii inajitokeza katika dondoo lifuatalo:

‘Kasekesi binti yangu, siku moja ijayo utaolewa. Sisemi ni lazima mwanamke aolewe. La! Lengo kuu la mwanamke maishani si kuolewa! Lakini ikiwa utaolewa, uusikilize ushauri wangu. Mtafute mwanamume ambaye anakuheshimu kama kiumbe, anayekuthamini kama kiumbe mwenye hisia na hisia kama hujui ni chanzo cha uhai wenyewe.’ *Unaitwa Nani?* Uk. 43

Dondoo hili linarejelea ushauri anaopewa Kasekesi na mamake ambapo anamhimiza kuhusu kumteua mwanamume atakayemheshimu iwapo angeamua kuolewa. Mawaidha haya yanakisi misingi ya Ufeministi Mamboleo unaosherehekea heshima na hadhi ya mwanamke katika jamii. Mamake Kasekesi anakataa dhuluma katika ndoa na kuhimiza bintiye kutafuta mchumba watakaye heshimiana na kupendana ili kuendeleza umoja katika ndoa. Hali hii inapolinganishwa na jamii ya Nana kuna usigano kwa vile katika jamii ya Nana mwanamke hana usemi au uamuzi kwa maswala ya unyumba. Jamii ya Nana inahimili dhuluma za kijinzia zinazosababisha ndoa nyingi kuvunjika kutokana na ubabedume unaohimizwa na mifumodume.

Mwandishi anamsawiri Nana kama mke mkombozi aliye na urazini kuhusu haki yake na yuko tayari kupigana kwa jino na ukucha kuitetea na kupinga dhuluma za kijinsia. Nana anasimama kidete na kukataa kuteuliwa mwanandoa, aliibuka kuwa mwanaufeministi mamboleo imara kwani alijichagulia mchumba wake Amour na wakaishi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2024

kwa amani na upendo. Hali hii inaakisiwa katika dondoo hili:

'Ndiye chaguo lake Nana, Amour. Ndiye aliyemtaka. Hakupagazwa naye tu. Hakulazimishwa naye. Wametafutana, wamefukuzana mbio kwa masafa ya mbingu na ardhi. Wametazamana kwa mbali kwa miaka hadi wakakutana..... Hatimaye wamejadiliana na kukubaliana kuanzisha ndoa ya kisasa.' Nyuso za Mwanamke, uk. 239

Dondoo hili linaonyesha kuwa Nana na Amour walikuwa na nafasi nzuri ya kujichunguza na kisha kuchaguana kama wanandoa kwa mujibu wa upendo wao. Hali hii inaafikiana na mawazo ya Nadharia ya Ufeministi Mamboleo ambayo inatetea haki ya mke kufanya uamuzi wa kibinafsi kuhusu maisha yake. Nadharia hii inahimiza ridhaa na hiari katika kufanya uamuzi unaomhusu mke. Mwandishi anahimiza wanandoa kuelewana na kukubaliana kuendeleza maisha yao kwa pamoja bila ya shuruti kutoka kwa mtu yeyote maana misingi ya ndoa imo katika mapenzi baina ya wanandoa wenyewe.

Katika jumuia inayosawiriwa kwenye riwaya *'Nyuso za Mwanamke',* wanawake hawakurithishwa mali ya wazazi wao na iwapo mzazi angekosa mtoto wa kiume, watoto wa nduguye ndio wangerithishwa mali hayo. Dhuluma hii ya kumnyima mwanamke haki ya kurithi mali ya wazazi inadhirika bayana katika dondoo lifuatalo:

'...kwa sababu wanawake saba hao waliozaliwa wasingelirithi mali nyingi ya baba yao iliyokuwa haina mipaka. Badala yake mali ingekwenda kwa mtoto au watoto wa kiume wa ndugu wa kiume wa baba mtu.' *Nyuso za Mwanamke*, uk. 108

Mhusika anayetajwa katika dondoo alikuwa na watoto saba wa kike na wasioweza kurithishwa mali maridhawa aliyokuwa nayo na kulazimika kutafuta mtoto wa nane ambaye angerithishwa mali, iwe ni wa kike au kiume. Nadharia ya Ufeministi Mamboleo inahimiza usawa na hivyo kukiuka misingi ya mfumodume wa kiuchumi ulioshenezwa katika utamaduni unaomkweza mtoto wa kiume na kumtweza mtoto wa kike. Nadharia ya Ufeministi Mamboleo inatambua haki ya mtoto wa kike kurithishwa mali ya wazazi wake sawa na mtoto wa kiume. Mwandishi anakashifu hali ya kumbugua mtoto wa kike kiuchumi. Badala yake anapendekeza usawa katika kuwarithisha watoto bila kujali jinsia. Usawa huu utaendeleza mshikamano katika familia kwa sababu warithi wanapokaa pamoja na kusemezana ndivyo jamii mpya yenye maelewano inakuzwa na kujengeka. Kwa hivyo, mwandishi anapendekeza kuwa, ni vyema kuwachana na mila zinazoendeleza tamaa ya kumpendelea mwanamume kwani mfumodume wa aina hii umepitwa na wakati.

Kwa upande mwingine, katika riwaya, '*Unaitwa Nani?*' taswira inayojitokeza inakinzana na ile ya jamii ya *Nyuso za Mwanake*. Kasekesi anashauriwa na mamake kuwa ateue mume asiyezingatia utamaduni uliopitwa na wakati. Wosia huu wa mzazi unabainisha mke aliye na urazini wa kiakili kuhusu haki ya mtoto wa kike katika jamii inayohimili mifumodume inayomdhulumu mwanamke. Hali hiyo inajitokeza katika dondoo lifuatalo:

'Mtafute mwanamume asiyetawaliwa na utamaduni usiofaa. Utamaduni ni kitambulisho muhimu cha mwanadamu lakini nao utamaduni sio jabali linalokwama pale pale; hubadilika kama mmea unaokua.' *Unaitwa Nani*, uk. 44

Jamii mbalimbali hutofautiana katika hali ya kumpa mwanamke nafasi ya kuwasilisha mawazo yake. Kuna zile zinazotoa nafasi hiyo na nyingine zinazompunja na kumuwekea vikwazo vinavyoendeleza dhuluma za kijinsia. Wosia wa mamake Kasekesi kwa bintiye unaakisi chembe za mawazo ya Nadharia ya Ufeministi Mamboleo kuhusu umuhimu wa kukata pingu zinazomfunga mwanamke kupitia kwa utamaduni na asasi za kijamii zinazosheheni mifumodume. Kupitia kwa nasaha anayoitoa kwa mwanawe mwenzake, anajimpambanua kimawazo na kumhamasisha kukataa maisha ya kudhulumiwa na jamii inayompendelea mwanamume. Anaendelea kusema kuwa licha ya utamaduni kuwa muhimu, haufai kuwa jabali kwani mazuri yatashikiliwa na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2024

yanayokiuka uhuru wa kijinsia yatupiliwe mbali kujikwamua kutoka kwa utumwa wa ubabedume.

Hali inaonekana kuwa tofauti katika jamii inayosawiriwa kwenye riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*. Katika jamii hiyo, utamaduni umempa mwanamume nguvu nyingi dhidi ya mwanamke. Kwa mfano, sheria za kitamaduni zinazoasisiwa na wanaume zinampendelea mwanamume na hivyo kuchunga na kuendeleza maslahi yake huku mwanamke akifinyiliwa na kudhulumiwa na sheria hizo. Usemi wa Nana katika dondoo lifuatalo unatoa taswira ya hali hii:

'Maisha yetu wanawake hapa petu yamefinyangwa ndani ya tamaduni zilizoasisiwa na mwanamume ambazo bado zina nguvu kubwa kupita kiasi. Zinafanana na tamaduni za *the untouchable* ambamo waliozaliwa vinyozi wanabaki vinyozi...' *Nyuso za Mwanamke*, uk. 107

Sauti ya Nana katika dondoo hili inapiga mwangwi sauti ya wanawake wote katika jamii yake wanaosikitikia utamaduni dhalimu ulioasisiwa na wanaume ili kuwakandamiza. Nana anapoangazia maisha ya mwanamke katika jamii yake, anaona kuwa amefinyiliwa kimabavu na utamaduni ulioanzishwa na mwanamume. Utamaduni huo unampa mume nguvu, uwezo na mamlaka kumdhibiti na kumkandamiza mwanamke. Nana anaapa katu kutofinyiliwa na utamaduni huo kama mamake wa kambo bali atapigana kwa jino na ukucha ili kujikomboa. Nana anaziita sheria za mwanamume kwa vile zimehimili ubabedume unaompendelea mwanamume na kumpa kipaumbele kwa kila jambo. Kimsigi, sheria hizo zimetungwa na mwanamume ili kumdhibiti mwanamke. Hali hii inazua jamii yenye ubaguzi inayopendelea mume na kutweza mke, hiki ndicho chanzo cha dhuluma za kijinsia zinazotokana na migogoro isiyo na kikomo baina ya mume na mke katika jamii. Nadharia ya Ufeministi Mamboleo inapinga ubaguzi wa aina yoyote kwa misingi ya kijinsia. Nadharia hii inapigania ujenzi wa jamii mpya yenye usawa wa kijinsia.

Kwa upande mwingine, Kasekesi naye anashauriwa katika '*Unaitwa Nani?*' kuwa kuna mambo ambayo wanaume wafaa kuona yamepitwa na wakati na kuyaachilia ili wasiwadhulumu wanawake. Mama anamshauri kuwa:

'Mtafute anayejua kuwa kuna mambo yanayopaswa kuachwa nyuma kwa sababu yamepitwa na wakati na asiyeongozwa na sauti ya kale inayopuma kwenye ubongo wake kama chungu cha maboga.......' Unaitwa Nani, uk. 44

Mamake Kasekesi alikuwa anaendeleza nadharia ya Ufeministi Mamboleo kwa kumhimiza kuwa atafute mwanamume anayeweza kuelewa mapisi ya wakati na kuyaacha mambo ambayo yanazua ukandamizwaji wa kijinsia ili kuendeleza umoja na ushirikiani katika jamii. Pia alitaka ateue mwanamume atakayeweza kumsikiliza na kuwafanya washauriane katika kufanya mambo ili kuondoa mapuuza yanayoendelezwa na ubabedume kisha kujenga jamii mpya yenye amani.

Kwa mujibu wa utamaduni katika *'Nyuso za Mwanamke'*, mwanamke alichukuliwa kuwa mali ya jamii na hivyo kuwa mtumishi kwa jamii nzima. Hali hii inaakisiwa katika dondoo lifuatalo:

Sadiki ...... hakunifanya mke tokea mwanzo. Alinifanya mtumishi tu wa kuipikia familia yake kubwa, familia nzima ambayo ina zaidi ya watu wanane watu wazima....... na si kupika tu, bali kufua, kupiga pasi, kufagia, kutandika na kutandua. Na labda hayo hayakuwa makubwa, Sadiki alitaka........' *Nyuso za Mwanamke*, 211

Shemsa alisimulia kwa kwikwi alivyofanywa kuwa mtumishi wa jamii baada ya kuozwa kwa lazima kwa Sadiki. Hii inabaini alivyodhulumiwa katika ndoa badala ya kuifurahia ndoa yake na Sadiki iliyoelekea kwa talaka kwa kushindwa kuvumilia kutumikishwa. Hii inakiuka madai ya Nadharia ya Ufeministi Mamboleo na kusisitiza ubabedume katika jamii ambayo mke hana usemi kwa kuwa mwanamume ndiye amepewa uwezo wa kusema na kufanya maamuzi apendavyo.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2024

Katika riwaya ya '*Unaitwa Nani?*' mwanamke vilevile anachukuliwa kuwa mali ya jamii, utamaduni uliruhusu mwanamke aweze kurithiwa na mume mwingine wakati mumewe wa kwanza ameaga. Hali hii inaakisiwa katika dondoo lifuatalo:

'Siku moja pakaja kundi la wazee limefuatana na wanaume wane;...akakumbushwa utamaduni ambao anaujua tangu hapo. Akaambiwa hao wanaume wamejia moja pale kumrithi.' *Unaitwa Nani?* Uk. 81

Nyakor ilifaa arithiwe na mwanamume mwingine kwa mujibu wa utamaduni wa jamii yao. Kwa kuwa hii ilikuwa dhuluma kwa mwanamke, Nyakor hakukubali iliyozua mgogoro baina yake na wale wazee. Huu ni utamaduni uliopitwa na wakati na ambao unafaa kuachwa maana unapotekelezwa utakuwa unaendeleza dhuluma kwa mwanamke na huo ni ubabedume.

**Dhuluma ya Kijinsia katika Ndoa**

Katika *'Nyuso za Mwanamke',* wanawake wengi wamekosa uhuru katika ndoa zao na kuwa wategemezi kwa waume wao inayoendeleza ubabedume maana wamedhibitiwa na waume zao. Kwa mfano, Nana anasema kuwa:

'...sitaki mimi kamwe hata kuwa mwanamke kwa maana ya mwanamke anayetunzwa na kulindwa na mwanamume kama mamangu wa kambo, au mwanamke hohe hahe anayefyonzwa damu taratibu huku akimalizika kama alivyomalizika mamangu mzazi.*' Nyuso za Mwanamke*, uk. 107

Usemi huu wa Nana unaonyesha kuwa wanawake wanakosa namna ya kujiendeleza kwa kudhibitiwa na waume zao. Ufeministi mamboleo unasisitiza uhuru wa mwanandoa wa kufanya maamuzi ambapo mwanamke akikubali kukaa nyumbani na kulea watoto aweze kulipwa kwa kazi hiyo. Iwapo hatakubali kukaa nyumbani ana uhuru wa kuajiriwa popote pale kama mwanamume. Udhibiti wa mwanamke huendeleza ubabedume ambao ni dhuluma ya kijinsia.

Katika riwaya *'Unaitwa Nani?',* wanawake pia wamenyimwa uhuru wao kwa hali tofauti tofauti. Taswira hii inajitokeza katika dondoo lifuatalo:

'....hapo ndipo niliposikia kile kisa cha profesa mmoja– nadhani aliitwa kitu kama Puru la pesa– wa chuo kikuu aliyemwoa mwanamke mdogo wa umri, aliyeishia kumwacha kwa kuubana uhuru wake.' *Unaitwa Nani?* Uk. 51

Masimulizi haya ya Kasekesi yanabainisha dhuluma kwa kuwa wanawake wananyimwa uhuru wa kutekeleza wajibu wao. Wanaume wanaamua kuwafungia nyumbani bila kutambua kuwa hiyo ni dhuluma ya kijinsia inayoendelezwa. Isitoshe, wanaume hawataki kuwaona wake zao wakifanya maendeleo ya kiuchumi ambayo yatawasaidia kujitegemea. Ndipo Kasekesi anasema kuwa:

'....atakubali mkewe afanye biashara na marafiki zake wamkejeli kwa kushindwa kumlisha mkewe. Unajua tena hawa wanaume wetu hawataki kumwona mwanamke anajitegemea kiuchumi.' *Unaitwa Nani?* uk. 54

Kasekesi aliwaza na kuwazua kisha akaamua kufungua biashara ili kukimu mahitaji yake ya kiuchumi iliyomletea nafuu katika ndoa yake. Ufeministi Mamboleo unahimiza wanawake kujitahidi na kukimu mahitaji yao ya kiuchumi ili kupunguza utegemezi kwa mwanamume linalozua ubabedume na kisha dhuluma ya kijinsia.

Katika *'Nyuso za Mwanamke'*, mwanamke amedharauliwa na mumewe katika ndoa na hataki kuusikiliza ushauri wowote kutoka kwa mwanamke. Kwa mfano, Bi Mau anapomhadithia Nana kuhusu mume aliyekiuka maelekezo ya mkewe:

'Tusimwoze binti yetu mtu wa mbali kwa ajili ya mapenzi yetu, tumwoze kwa mapenzi yake, hata kama mposaji ni mkwasi wa matajiri wote duniani. Mwanamume akakataa hawakumwona tena maishani mwao, kwani huko alikochukuliwa alifungiwa na hata wazee wake wakazuiwa kumtembelea.' *Nyuso za Mwanamke*, uk. 69

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2024

Masimulizi haya yanaonyesha kuwa dharau la mwanamume kwa mwanamke huweza kumponza hata yeye mwenyewe. Mwanamume huyu alipokaidi maoni ya mkewe ya kutomwoza bintiye kwa kutaka mali, waliweza kuzuiwa wote wasimwone binti wao wala binti kuwatembelea. Ufeministi Mamboleo unahimiza ushirikiano na uelewano katika kufanya maamuzi na iwapo lingezingatiwa hakungekuwa na tatizo hili linalosababisha utengano wa binti na wazazi wake hata kukosa kuonana. Kwa hivyo, tamaa ya mali inachangia katika kuendeleza ubabedume unaozua dhuluma za kijinsia maana mume amemzuia mkewe kuonana na wazazi wake baada ya kumwoa lililo kinyume katika haki za kibinadamu.

Kwa upande wake, riwaya ya *'Unaitwa Nani?'* inadhihirisha kuwa mwanamke anadhulumiwa katika ndoa na jamaa za mumewe anapoaga na kulimbikiziwa lawama si haba. Kasekesi aliweza kushangaa na aliyoyaona baada ya kifo cha mumewe. Hali hiyo inaakisiwa katika dondoo lifuatalo:

'Kwetu mwanamke anapoolewa anakuwa adui wa jamaa za mumewe; ni kama amewatoa nyama kinywani! Mambo yalianza siku moja kabla mazishi nilipigwa na mshtuko. Jamaa zake Agusto walisema kuwa nilihusika katika kifo chake. Kwamba mimi ni mchawi, usiku huo nililazimishwa kulala chumba kimoja na maiti ya mume wangu.' *Unaitwa Nani?* Uk. 57

Haya ni madhila kwa mwanamke yanayodhihirisha kuwa mke ni mali ya jamii nzima na aweza kufanyiwa lolote hata mumewe anapoaga na hivyo kuendeleza dhuluma ya kijinsia. Mwanamke pia anadharauliwa katika riwaya ya *'Nyuso za Mwanamke'* kwa kupigwa na mumewe kama ishara ya kumrekebisha. Dondoo lifuatalo linatoa picha ya hali hiyo:

'Ukelele wa bibi mmoja aliyekuwa akipigwa na mumewe kwa kuchelewa kumtayarishia uji wa kisabeho.' *Nyuso za Mwanamke*, uk 75

Maelezo haya ya Nana yanaonesha vile mwanamke anadharauliwa na kudhulumiwa kwa kupigwa kwa sababu hili ni jambo ambalo wangesuluhisha kwa kuzungumza. Hii inaendeleza ubabedume katika jamii na hivyo kuhahalisha dhuluma ya kijinsia. Katika '*Unaitwa Nani?'*, mwanamke pia anadhulumiwa kwa kupigwa na mumewe katika ndoa. Dondoo lifuatalo linatoa picha kamili:

'......siku moja nilipomwona mama akitoka kwenye chumba chao cha kulala akiyapangusa machozi muda mfupi baada ya kumsikia baba akiguta humo ndani kama fahali aliyefungiwa zizini. *Unaitwa Nani?* Uk. 42

Kasekesi alipoambiwa kuhusu ndoa, aliweza kukumbuka alichokiona kwa mama yake na kuwa na wasiwasi iwapo ndoa yake ingekuwa vile au la. Alikumbuka mamake akilia kwa kupigwa na hivyo akatambua hali ya ubabedume inayoweza kutokea katika ndoa yoyote ile.Isitoshe, wanawake walizuliwa kuajiriwa hata kama wamesoma na kubakia wategemezi kwa waume zao kama namna ya kuwadhibiti. Hili linaakisiwa katika dondoo lifuatalo:

'....Mimi nilikuwa na hakika kwamba kwa aina ya mume anayetaka kunioa ningekuwa mtawa tu. Nisingeliruhusiwa kufanya kazi niliyoisomea kwa juhudi na kutazamia kupata kipatochangu mwenyewe ambacho kingenipa uhuru na kuniwezesha kujitegemea kwa namna fulani.' *'Nyuso za Mwanamke'*, Uk 210

Kwenye kipindi cha dukuduku, wanawake walikuwa wakielezea madhila waliyokumbana nayo maishani ndiposa Shamsi akaelezea hofu zake kwani mwanamke alikuwa haruhusiwi kuajiriwa bali kukaa nyumbani. Hali hii inakiuka madai ya Nadharia ya Ufeministi Mamboleo inayowapa wanawake nafasi sawa na wanaume hata katika ajira na kupinga ubabedume unaomdhibiti mwanamke. Vivyo hivyo, katika '*Unaitwa Nani?'*, mwanamke hakutakiwa kuonekana akijiendeleza kiuchumi au kufanya kazi inayompa pesa na kujitegemea kwani wanaume wanaona kuwa hawangeweza kuwadhibiti. Dondoo lifuatalo linatoa picha ya hali hiyo:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2024

'Unajua tena hawa wanaume wetu hawataki kumwona mwanamke anajitegemea kiuchumi.' *Unaitwa Nani?* Uk 54

Maelezo haya ya Kasekesi yanaonyesha kuwa wanaume wengi hawataki kuwaona wake zao wakiajiriwa au kujiendeleza kiuchumi ili kuwafanya wasalie wategemezi kwao na hivyo kuwadhulumu wapendavyo. Huu ni ubabedume wa hali ya juu na hivyo ufeministi mamboleo kuhimiza wanawake kujitahidi ili kujitafutia uhuru wao kiuchumi.

Mwanamke anadhulumiwa katika ndoa ya lazima na mumewe pamoja na wanajamii. Tunamwona Bimkubwa akifungwa kwa kamba ndipo mumewe aweze kula soro kwa sababu ya kulazimishiwa mume asiyempenda. Hili linaakisiwa katika dondoo lifuatalo:

'.... walikuja kunifunga miguu na mikono, na kunizamisha kitambaa kinywani. Nikabaki kubanikwa kama kuku wa kupaka, mguu huku na mguu kule, na hapo ndipo bwana alipokula soro na kuniacha na kidonda cha ndani kwa ndani ambacho hakikupona wala hakitapona milele....' *Nyuso za Mwanamke*, uk 236

Hapa Bimkubwa anaelezea shida alizozipata baada ya kulazimishiwa mume ambaye hakumpenda. Alijaribu kupigana lakini akaambulia patupu maana jamii ililazimisha na kufuatilia iliyozua dhuluma katika ndoa maana walimsaidia Bwana Hila kumbaka mkewe, Bimkubwa. Hii inakiuka ufeministi mamboleo unaohimiza ndoa ya wapendanao huku ikiendeleza ubabedume kwa kumpendelea mwanamume huku mwanamke akidhulumiwa kwa kulazimishiwa asiyemtaka. Katika *'Unaitwa Nani*?', mwanamke pia anadhulumiwa kwa kuchukuliwa kuwa adui wa jamii ya mumewe anapoolewa. Hali hii inaakisiwa katika dondoo lifuatalo:

'Kwetu mwanamke anapoolewa anakuwa adui wa jamaa za mumewe; ni kama amewatoa nyama kinywani!' *Unaitwa Nani?* Uk. 57

Kasekesi alipopeana habari za kifo cha mumewe kilichosababishwa na matatizo ya ini kupitia ulevi kupindukia, yeye alishukiwa na jamaa za mumewe kuwa amemuua mumewe. Wakaongezea kuwa yeye alikuwa mchawi ambayo yalimshangaza na kumfanya kupigwa na butwaa. Baada ya hayo aliadhibiwa na jamii hii kwa namna mbalimbali ikiwemo kulala na maiti ya mumewe katika chumba kimoja. Hii ni dhuluma kwa mwanamke inayoendelezwa na ubabedume unaoshikiliwa na jamii nyingi ili kuonyesha kuwa mwanamke hana lolote la kujitetea nalo. Hawa katika *Nyuso za Mwanamke*, analilia mtoto wake wa kike aliyeuawa na mumewe tu baada ya kujifungua mtoto wa kike.

'....Kitoto nilikiona kwa jicho langu nilipokuwa nikikizaa. Chanajike, kitipwatipwa, kina siha yake kamili. Wakaninyang'anya kwa nguvu........ wakaingia nacho mwituni huku kinalia kilio kikali. Waliporudi wakaniambia kimekufa....... Wamekiua,...... kwa nini wasiniachie mwenyewe?.......' Nyuso za Mwanamke, Uk. 180

Hawa analilia kitoto chake kilichouawa kwa kuwa ni cha kike na ndiposa anatamani heri angeachiwa yeye mwenyewe ashughulike nacho. Ndiposa Nana anamsihi kuwa anyamaze maana haki itatendeka. Hii ni dhuluma maana watoto huzaliwa wa kike na kiume na wote wana haki ya kuishi. Nadharia ya Ufeministi Mamboleo inakashifu dhuluma zozote zile yakiwemo mauaji kwa mujibu wa jinsia.

**Dhuluma ya Kijinsia katika Elimu**

Wanawake wameweza kuhujumiwa kielimu kwa kunyimwa nafasi za kuendeleza masomo yao kwa hali mbalimbali. Kwa mfano katika riwaya *'Unaitwa Nani?'*Mwanamuka anaozwa na wazazi wake kutokana na umaskini uliokithiri. Walipotaka usaidizi kwa wanajamii wakaona huko ni kujisumbua tu na kupoteza muda:

'Ya nini kujisumbua? Mtoto wa kike unamwelimisha nini na ataishia kuolewa? Umesikia wapi mtu anatafuna nyama inayomezwa na mwingine?' *Unaitwa Nani?* Uk. 63

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2024

Hii inadhihirisha kuwa masomo ya mwanamke hayakuzingatiwa na wanakijiji wengi ndiposa wakakataa katakata kuwaauni wazazi wa Mwanamuka kuendeleza masomo ya mwana wao. Ufeministi Mamboleo unakataa msimamo huu wa wanakijiji kwani unasisitiza usawa katika kuhudumia jinsia zote kisawasawa.

Riwaya *'Nyuso za Mwanamke'* inasawiri hali tofauti kwa sababu mwanamke alisomeshwa licha ya kukumbana na changamoto tofauti. Nana aliweza kusomeshwa licha ya kutawishwa maana alipelekwa shuleni kwa gari na kurudishwa pia kwa gari bila kuruhusiwa kutangamana na kucheza na watoto wenzake:

'...... nilikuwa nikipelekwa na kurudishwa nyumbani kutoka shule kwa gari mojawapo miongoni mwa yale yaliyoendeshwa na madereva wetu........ akashikilia kwamba lazima anilinde. Lazima anihifadhi, hasa kwa vile bado ni msichana, sijapata mume.......' *Nyuso za Mwanamke*, uk 38

Babake Nana alikasirika sana Nana alipomwomba aende shule pekee yake ndiposa baba akamwambia kuwa yeye ni mtoto mdogo wa kike na ni sharti amlinde. Licha ya kuwa mtoto anafaa kulindwa, inapasa pia apewe nafasi ya kutangamana na wenzake ili kukua vyema kwani pia watoto wanahitaji usawa wanaposhughulikiwa katika jamii inavyosisitizwa na Ufeministi Mamboleo. Mbali na hayo, Nana hakuruhusiwa kucheza hata na watoto wengine; alitawishwa na babake:

'....tokea nilipokuwa mdogo, vitabu vimekuwa wandani wangu. Hasa mimi niliyeishi maisha ya upweke........... Isitoshe babangu hakutaka niwe na rafiki kutoka nje. Hakutaka nishiriki mchezo wowote nje ya nyumba yetu......' *Nyuso za Mwanamke*, uk 118

Licha ya kuwa Nana alipewa fursa ya kusoma vitabu vingi alivyonunuliwa na babake, alitawishwa na kumfanya aishi maisha ya upweke. Hii iliendeleza dhuluma kwa Nana maana mwanadamu anastahili kutangamana na wengine ili maisha yake kuwa vizuri; iliyodhihirisha ubabedume kutoka kwa babake Nana. Nana alijitahidi na kufanikiwa masomoni mwake hata kama alikuwa ametawishwa. Kwa upande mwingine, baadhi ya wazazi pia hawawaruhusu watoto wao wa kike kukamilisha masomo yao:

'Shule hakuwahi kuimaliza kama ndugu zake. Babake alisema kuwa elimu ndogo ya shule ya msingi ilimtosha.' *Unaitwa Nani?* Uk. 90

Kamene aliachishwa shule ili aozwe na yeyote aliyejaribu kumzungumzia babake kuhusu masomo yake, aligeuka kuwa pilipili. Hii ni dhuluma ya kijinsia maana mtoto wa kike ananyimwa uhuru wa kuendelea na masomo licha ya yeye kuwa mwanafunzi stadi shuleni. Huu ulikuwa ni ubabedume unaopingwa na ufeministi mamboleo unaopigania nafasi sawasawa kwa mtoto wa kike na wa kiume. Vivyo hivyo katika *'Nyuso za Mwanamke'*, Bimkubwa aliwachishwa shule katika darasa la kumi na mbili na kuozwa kwa lazima na babake:

'.... Bimkubwa.......shule ambako alisoma hadi darasa la kumi na mbili na baadaye kukatishwa masomo na kuingizwa chuo kikuu cha ndoa ya lazima.' Nyuso za Mwanamke, uk 290

Masomo ya Bimkubwa yalikatizwa kwa lazima kwa wazee wake kumwoza katika ndoa ambayo haikudumu. Huu ni ubabedume unaokandamiza jinsia ya kike na kufanya maisha yao kuzorota. Jambo hili linapingwa vikali na ufeministi mamboleo unaohimiza usawa wa kijinsia. Kwa upande mwingine, mtoto wa kiume hakufanyiwa lolote anapoacha shule kwa hiari badala ya kuhimizwa asome kwa bidii:

'Hata hivyo, shule aliiacha kabla ya kumaliza.' *Unaitwa Nani?*', Uk. 163

Dondoo hili linamrejelea kifungua mimba wa Pasta, Kenzi kwa kuacha shule bila maelezo yoyote. Hili ni kinaya kwani wanawake waliotaka kusoma hawakushughulikiwa na kisha kulazimishiwa ndoa za mapema ilhali wanaume wanaopewa kipaumbele kwa masomo wanayaacha bila sababu. Hii inaendeleza dhuluma

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2024

ya kijinsia inayopingwa na ufeministi mamboleo kwa kuhimiza usawa katika kushughulikia jinsia zote.

## Hitimisho

Makala hii imejadili dhuluma mbalimbali za kijinsia zinazoibuka kutokana na riwaya teule, *'Nyuso za Mwanamke'* na *'Unaitwa Nani?'* katika vitengo mbalimbali. Riwaya hizi zimeibua kuwa jinsia ya kike ndiyo inayodhulumiwa sana katika jamii inayompendelea mwanamume. Madhila yanayompata mwanamke katika sekta mbalimbali za maisha yanamfanya kuanza kufunguka macho ili aelewe zaidi jamii anamoishi na kuchunguza sababu ya kudhulumiwa kwake. Kwa hivyo, taasisi mbalimbali zinazomdhulumu mwanamke kiutamaduni, kwenye ndoa na hata kielimu zinadhihirika.

Nadharia ya Ufeministi Mamboleo pamoja na ile ya Hegemonia ya Ubabedume zinasaidia katika kuelewa namna dhuluma mbalimbali zinaendelezwa na kisha kudhihiri vyanzo vya dhuluma hizo. Nadharia hizi zinahimiza usawa wa kijinsia katika misingi ya maisha ili kuijenga jamii mpya yenye amani na utulivu.

## Marejeleo


Chimerah, R. & Njogu, K. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

DuBois, E. C. (1997). *Harriot Stanton Blatch and the Winning of Woman Suffrage*. New Haven, Conn.: Yale University Press.

Flexner, E. (1996); Century of Struggle: The Woman's Rights Movement in the United States. The Belknap Press.

Goodman, R. T. (2010). *Feminist Theory in Pursuit of the Public: Women and the 'Re-Privatization' of Labor*. New York: Palgrave Macmillan.

Kibigo, M. L. (2019). *Ubabedume katika Majigambo ya Miviga ya Shilembe na Mchezaji wa Mayo ya Wahusika Nchini Kenya Kwa Mtazamo wa Kisemantiki*. (Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Masinde Muliro) Kakamega, Kenya.

Malenya, M. M. (2012). *Matumizi ya Lugha katika Fasihi Simulizi*. Mwanza: Inland Press.

Masibo, B. (2009). *Gendered Perspectives in Novels of Ngugi wa Thiong'o and Walker A*. (Phd Thesis, University of Nairobi. Unpublished).

Njogu, K. & Wafula, R.M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Pilcher, J. & Welchan, M. (2004). *Fifty Key Concepts in Gender Studies*. London: Sage Publications.

Beauvoir S.(1949). The Second Sex. London: Pan Books Publishers.

Nyangweso M. S.(2017). Nafasi na Athari za Kiongozi wa Kike katika Tamthilia Teule za Kiswahili. Tasnifu; Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

Mboya L.A. (2018). Dhuluma kama Kichocheo cha Mzinduko wa Mwanamke Katika Riwaya ya Kiswahili.

Khamis S. A. (2012). 'Riwaya Mpya ya Kiswahili. Utandawazi au Utandawazi? Jinsi Lugha ya Riwaya mpya ya Kiswahili Inavyodai.' Bayreuth University.

WHO (2020) World Report on Gender Based Violence. Geneva: World Health Organisation


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.